# AckySHINE.com

# Je, baada ya kutumia vidonge au sindano kwa muda mrefu, mwamamke akiacha kuzitumia hizo njia ataweza kupata mimba tena?

By SW - Melkisedeck Shine · April 16, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Vidonge na sindano zinazuia mimba kwa kuzuia yai lisipevuke. Akitumia njia hizi za kuzuia mimba, mwanamke anaona hedhi yake kama kawaida, lakini hakuna yai linalokuwa limepevuka kwa ajili ya kurutubishwa. Mara mwanamke akiacha kutumia vidonge, mayai hupevuka tena ndani ya kokwa na mwanamke huweza kupata mimba. Mwanamke aliyetumia sindano, anaweza akachukua muda kiasi kurudia hali yake ya uzazi. Kwa wanawake wengine inachukua miezi 12. Muhimu ni kukumbuka kwamba sindano na vidonge siyo njia za kudumu za kuzuia mimba, hata kama itachukua muda fulani kurudia hali ya kawaida ya uzazi